

Kama ni msomaji wa biblia, Neno hilo utakutana nalo katika baadhi ya vifungu kwenye Zaburi..

### Zaburi 11:2

*[2]Maana, tazama, wasio haki wanaupinda uta, Wanaitia mishale yao katika upote, Ili kuwapiga gizani wanyofu wa moyo.*

### Zaburi 21:12

*[12]Kwa maana utawafanya kukupa kisogo, Kwa upote wa uta wako ukiwaelekezea mishale.*

Upote ni ule uzi mwembamba unaofungwa kwenye uta, ambao mishale huwekwa pale kwa kuvutwa na kurushwa.

Upote hutengenezwa kwa ngozi na wakati mwingine kamba za mimea

imara.. ni lazima utengenezwe kwa malighafi imara, ili isikatike pale unapovutwa.

Kwasababu hizi ni zana za kivita...kiroho hufunua pale mbili. Adui hutengeneza upote wake, ambao hurushia watu mishale ya moto ili kuwaua kiimani (Waefeso 6:16), ili kuweza kuishinda, biblia inatufundisha daima tuibebe ngao ya Imani.

Lakini pia Bwana Yesu anao upote wake ambao kwa huo hutupa silaha zake kwa adui zetu, sawasawa na hiyo Zaburi 21:12, Na silaha za Kristo zina nguvu sana sio tu kumlenga adui lakini pia kuangusha ngome.

Maboma na makao ya shetani.

2 Wakorintho 10:4-5

*[4](maana silaha za vita vyetu si za mwili, bali zina uwezo katika Mungu hata kuangusha ngome;)*

*[5]tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo;*

Lakini Nguvu ya silaha hizi hutegemea na hali ya mtu kiroho katika maeneo matatu;

1) kimaombi,

2)Utakatifu

3) Injili.

Mwamini wa namna hii ambaye huchukia dhambi, huubiri injili na huzingatia kudumu katika maombi ya masafa,

Kiroho ni askari imara na mwenye silaha zenye nguvu sana, ziwezazo kumuharibu ibilisi.

Kuwa askari kamili wa Kristo

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako

bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

Mtambo/mitambo ni nini kibiblia?

Na kipenu ni nini (Isaya 1:8)

Kutawa ni nini? Sawasa na Luka 1:24

Share on:  
WhatsApp

Print this post